



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



SIMU NA.0737235630

Email- ded.itigidc@singida.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi
01 Barabara ya Halmashauri
S.L.P 70,
43483 ITIGI - SINGIDA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HW/ITG/S1/22 VOL III/127

13 Julai, 2023.

Kwa wananchi wote

KURUDIA TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika mwaka wa fedha 2022/2023 yenye Kumb.Na. FA.97/228/01'TEMP/06 cha tarehe 06 Aprili, 2023 Kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anarudia kuwatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa ya kuomba nafasi ya kazi iliyotangazwa hapo chini.

1. MWANDISHI MWENDESHA OFISI (KATIBU MAHSUSI) DARAJA LA II – (NAFASI 2)

Kazi na Majukumu ya Mwandishi Mwendesha Ofisi

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anapofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake Majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

Sifa za Mwombaji

- Awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) mwenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au Cheti cha NTA Level 6 ya Uhazili.
- Awe amehudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya tatu
- Awe amefaulu Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Powerpoint, Microsoft office, Internet, E – mail na Publisher.

Mshahara

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani **TGS C** kwa Mwezi

1. MASHARTI KWA UJUMLA

- Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka arobaini na tano (45)
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe na maelezo yao binafsi (C.V)
- Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha (IV na VI), na picha moja ya rangi katika barua ya maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- **"Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (FORM IV and FORM VI RESULT SLIPS) HAVITAKUBALIWA**

- Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **27 Julai, 2023** saa **9:30** Alasiri

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi
01 Barabara ya Halmashauri
S.L.P 70,
43483 ITIGI - SINGIDA.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:



John K. Mgalula

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.

- Mbao za Matangazo

